**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA**

# IJUE SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI NA KANUNI ZAKE

Imeandaliwa na:
Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa
Viwanja vya Nanenane Nzuguni
Jengo la Wizara ya Kazi - Mtaa wa Nzuguni A
S.L.P. 2851
**DODOMA**.

**Toleo la Julai, 2020**

# YALIYOMO


1.0 UTANGULIZI ........................................................................................................ 1

2.0 LENGO LA SHERIA ...................................................................................... 1

3.0 MSIMAMIZI WA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI ..................... 1

4.0 GHARAMA ZA UCHAGUZI ......................................................................... 2

5.0 UWAZI WA MAPATO NA MATUMIZI ........................................................... 3

6.0 MENEJIMENTI YA GHARAMA ZA UCHAGUZI ..................................... 4

7.0 TIMU YA KAMPENI ..................................................................................... 5

8.0 VIWANGO VYA GHARAMA ZA UCHAGUZI ......................................... 6

9.0 MGAWANYO WA MATUMIZI BAINA YA CHAMA NA MGOMBEA....... 8

10.0 MAREJESHO YA GHARAMA ZA UCHAGUZI ......................................... 8

11.0 UKAGUZI WA GHARAMA ZA UCHAGUZI ............................................. 9

12.0 VITENDO VINAVYOKATAZWA .......................................................................9

13.0 ADHABU CHINI YA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI...............12

14.0 UTARATIBU WA KUWASILISHA MALALAMIKO................................. 14

15.0 WAJIBU WA MTU KUTOA TAARIFA KUHUSU UKIUKWAJI WA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI NA KUMLINDA MTOA TAARIFA..... 15

16.0 HITIMISHO................................................................................................ 15

4. Kuepuka vitendo vya vurugu na rushwa katika uchaguzi.

Mafanikio ya utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi yanategemea ushirikiano wa viongozi na wanachama wa Vyama vya Siasa, wadau mbali mbali wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa, pamoja na wananchi kwa ujumla, hivyo wanapaswa kuisoma vema Sheria hii na kuitekeleza ipasavyo.



## 1.0 UTANGULIZI

Sheria ya Gharama za Uchaguzi Namba 6 ya mwaka 2010 ilitungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 11 Februari 2010 na kutiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17 Machi, 2010. Kabla ya Sheria hii kutungwa, nchi yetu haikuwa na mfumo maalum wa kusimamia na kuratibu gharama za uchaguzi kwa wagombea wa Vyama vya Siasa.

Wakati wa uchaguzi, kulijengeka utamaduni kwamba uongozi unaweza kununuliwa kwa fedha. Vilevile, tofauti ya uwezo wa kifedha wa wagombea ilikuwa kubwa kiasi ambacho baadhi ya wananchi walikuwa wakichagua viongozi kwa minajili ya uwezo wao wa kifedha na sio uwezo wa kuongoza na ubora wa sera za vyama vyao. Hivyo, Sheria hii inaimarisha demokrasia wakati wa uchaguzi kwa kuhakikisha kwamba kunakuwepo mazingira yaliyo sawa kwa wagombea na kudhibiti matumizi ya fedha wakati wa uchaguzi ili kupata viongozi bora.

## 2.0 LENGO LA SHERIA

Sheria ya Gharama za Uchaguzi imetungwa kwa malengo yafuatayo:-

1. Kutoa mwongozo wa mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa (kura za maoni) na kuusimamia kisheria;
2. Kuweka utaratibu wa kisheria wa kudhibiti gharama za uchaguzi;
3. Kuweka ukomo wa juu wa gharama za uchaguzi;
4. Kuweka utaratibu na mfumo wa uwajibikaji wa mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi.

## 3.0 MSIMAMIZI WA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI

Kifungu cha 4 cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi kimempa Msajili

wa Vyama vya Siasa wajibu wa kusimamia utekelezaji wa sheria hii na mamlaka yafuatayo:

1. Kufanya uchunguzi kuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi (Kifungu 5(1));
2. Kuhitaji taarifa zinazohusu utekelezaji wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi. (Kifungu 6(1)(2)); na
3. Kuwasilisha kwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi pingamizi dhidi ya mgombea aliyeshindwa kuweka wazi kiasi na vyanzo vya gharama za uchaguzi akiiomba Tume ya Uchaguzi kumwengua mgombea asiendelee kushiriki katika uchaguzi, baada ya kumsikiliza mgombea na kujiridhisha kuwa mgombea huyo anastahili kuenguliwa katika uchaguzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikishapokea pingamizi lililowasilishwa na Msajili wa Vyama vya Siasa inaweza kutoa amri ya kukiondoa chama au mgombea katika uchaguzi. (Kifungu cha 20(1-3)).

## 4.0 GHARAMA ZA UCHAGUZI

Gharama za Uchaguzi maana yake ni fedha au gharama zote zilizotumika kwa ajili ya kuendesha au kusimamia uteuzi wa wagombea ndani ya chama cha siasa, kampeni za Uchaguzi, mgombea na Serikali kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 7 (1) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi.

Gharama za uchaguzi zinajumuisha yafuatayo:

1. Gharama zote zilizotumiwa na chama cha siasa wakati wa mchakato wa uteuzi wa wagombea;
2. Gharama zote zilizotumiwa na chama katika kumdhamini mgombea wake;
3. Gharama zote zilizotumiwa na chama na mgombea wakati wa kampeni;
4. Gharama zote zilizotumiwa na Serikali, Chama cha Siasa na Mgombea wakati wa uchaguzi; na
5. Gharama zote zitakazotumika kwa ajili ya vikundi vya uhamasishaji kwa lengo la kumnadi mgombea kwa wapiga kura, gharama za chakula, vinywaji, malazi au usafiri ambazo mgombea amegharamia wakati wa kampeni.

Kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi kimeeleza kuwa, ni wajibu wa kila chama cha siasa kuendesha na kugharamia kampeniza



atayafanyia kazi ndani ya siku tano na kutoa taarifa ya uamuzi wake kwa wahusika na kutoa nakala ya uamuzi kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi na Katibu Mkuu wa Chama husika (Kanuni 18 na 19 ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi).

Endapo mgombea, wakala wake au kupitia chama chake atatenda vitendo vinavyokatazwa vilivyoanishwa katika Sheria ya Gharama za Uchaguzi, ikiwa hajachukuliwa hatua yoyote ya kisheria basi Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kufungua shauri la kosa la jinai au uchunguzi dhidi yake. Aidha, mtu aliyefanya vitendo vinavyokatazwa awe ameshinda au ameshindwa uchaguzi, anaweza kuwajibishwa kwa mujibu ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura ya 292 na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. (Kifungu 24(3) na (4)).

## 15.0 WAJIBU WA MTU KUTOA TAARIFA KUHUSU UKIUKWAJI WA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI NA KUMLINDA MTOA TAARIFA

Mtu yoyote atakayekuwa na taarifa juu ya kutendwa au kusudio la kutenda kitendo kilichokatazwa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi, atapaswa kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa. (Kifungu 13A(1) cha Sheria ya Vyama vya Siasa sura ya 258).

Sheria inamlinda mtoa taarifa, na haitokuwa lazima kwa shahidi kutaja jina au anwani ya mtoa taarifa katika kesi ya jinai au ya madai. (Kifungu 13A(2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa).

Mtoa taarifa yoyote atakayedhuriwa na mtuhumiwa wa vitendo vya rushwa au vitendo vilivyokatazwa, pamoja na washirika wake, baada ya Msajili wa Vyama vya Siasa kufanya tathmini juu ya kiwango cha madhara aliyoyapata, mtu huyo atapatiwa ulinzi, fidia na msaada wa Serikali. (Kifungu 13A(4) cha Sheria ya Vyama vya Siasa).

## 16.0 HITIMISHO

Sheria ya Gharama za Uchaguzi inasisitiza mambo yafuatayo:-

1. Uwazi katika mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi;
2. Uwajibikaji katika mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi;
3. Utunzaji wa kumbukumbu za gharama za uchaguzi; na

adhabu isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) na kwa taasisi yoyote itapewa adhabu isiyozidi shilingi milioni tano (5,000,000/=). (Kifungu 12(4) kikisomwa pamoja na kifungu 26).

13.7 Mgombea au wakala wake au kupitia chama chake atakayetenda vitendo vinavyokatazwa na Sheria ya Gharama za Uchaguzi atastahili kuenguliwa kushiriki katika uchaguzi au atashitakiwa kwa kutenda kosa la jinai kwa mujibu ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343, Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Sura ya 292 na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. Aidha, mgombea hatowajibika kwa kitendo kilichokatazwa kilichofanywa na chama chake bila idhini yake au makubaliano ya moja kwa moja au ya kimazingira. (Kifungu 24(1),(2),(3)).

13.8 Mtu yoyote atakayemzuia Msajili wa Vyama vya Siasa au mwakilishi wake kutekeleza wajibu wake chini ya sheria hii au atakayekataa kuwasilisha nyaraka mbalimbali zitakazohitajika na Msajili wa Vyama vya Siasa au kuwasilisha nyaraka au taarifa ya uongo au kutoa taarifa ya uongo katika marejesho au taarifa ya fedha au kuharibu nyaraka zinazohusiana na uchunguzi, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyozidi Shilingi milioni tano (5,000,000/=). (Kifungu 27).

13.9 Asasi ya kiraia au taasisi ya kidini itakayotumia fedha zaidi ya ukomo uliowekwa na Kanuni za Sheria ya Gharama za Uchaguzi au itakayoshindwa kuwasilisha programu ya mafunzo kwa Msajili wa Vyama vya Siasa au programu yake ya mafunzo ikitumika kubagua mgombea au chama cha siasa itakuwa imetenda kosa la jinai na ikitiwa hatiani itawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano (5,000,000/=). Kanuni ya 12 ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi ikisomwa pamoja na Kifungu 26(c ) cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi.

## 14.0 UTARATIBU WA KUWASILISHA MALALAMIKO

Mtu yoyote atakayekuwa na taarifa ya uvunjifu wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi anaweza kuwasilisha taarifa au malalamiko yake kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kwa maandishi akionesha kitendo kilichofanywa au ambacho hakikikufanyika kinachohusu malalamiko hayo na ushahidi wake. Baada ya kupokea malalamiko hayo, Msajili wa Vyama vya Siasa



uchaguzi kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato. Hata hivyo, Kifungu cha 8(2) cha Sheria hiyo kinaruhusu mgombea kutumia fedha zake wakati wa kampeni pale inapobidi au anapolazimika kufanya hivyo.

## 5.0 UWAZI WA MAPATO NA MATUMIZI

Katika kudhibiti matumizi ya gharama za uchaguzi, Sheria ya Gharama za Uchaguzi imeweka sharti la kuweka wazi mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi ili kuhakikisha fedha zinazotumika zinatokana na vyanzo halali kisheria. Vilevile, Sheria hii imeweka sharti la uwazi katika matumizi ya gharama za uchaguzi kwa lengo la kuhakikisha kwamba matumizi yote ya gharama za uchaguzi yanafanyika kwa mujibu wa Sheria.

Katika kuhakikisha kunakuwa na uwazi katika mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi, Kifungu cha 9(1) na 13(1) kimeweka utaratibu kwa vyama vya siasa, wagombea, asasi za kiraia, na taasisi za kidini kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya gharama za uchaguzi kabla na baada ya uchaguzi. Taarifa hizo ni:

1) Kila mgombea aliyeteuliwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi anapaswa ndani ya siku saba (7) baada ya siku ya uteuzi kutoa taarifa ya gharama za uchaguzi (i) alizonazo, (ii) anazotarajia kupata na kuzitumia kama gharama za uchaguzi. Kwa upande wa mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano atatoa taarifa kwa Katibu Mkuu wa chama chake. Kwa mgombea ubunge au udiwani atatoa taarifa kwa Katibu wa Wilaya wa chama chake. Taarifa hizo zitakuwa katika fomu namba EE.1 na EE.2 kwa mujibu wa kanuni ya 9(1) na 13 ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi. Afisa aliyepewa mamlaka baada ya kupokea fomu za kuweka wazi gharama za uchaguzi ikiwemo fomu EE.1 na EE.2, ataziwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ndani ya siku saba baada ya siku ya uteuzi. Afisa aliyepewa mamlaka ya kupokea fomu za kuweka wazi gharama za uchaguzi kwa wagombea ubunge na udiwani ni Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo au Kata.

2) Kila chama cha siasa kitakachoshiriki uchaguzi, kitatakiwa ndani ya siku thelathini (30) baada ya uteuzi wa wagombea kufanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, kutoa taarifa ya fedha zote kinazokusudia (a) kutumia kama gharama za uchaguzi, na (b)

kutumiwa na wagombea wake kama gharama za uchaguzi.

3) Kila chama cha siasa kilichopokea mchango unaozidi Shilingi milioni moja kutoka kwa mchangiaji binafsi au Shilingi milioni mbili kutoka kwenye taasisi, kinapaswa kupitia bodi yake ya wadhamini kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ndani ya siku 30 baada ya kupokea mchango huo, kwa kujaza fomu EE.7 au EE.8. (Kifungu cha 11 (1)).

Katibu Mkuu au Katibu wa Wilaya wa chama husika akishapokea taarifa ya gharama za uchaguzi kutoka kwa mgombea atatoa cheti cha uthibitisho kwamba mgombea ametimiza masharti ya kutoa taarifa za gharama za uchaguzi. (Kifungu cha 9(4)).

Taarifa ya gharama za uchaguzi itakayotolewa na mgombea, pasipokuwa na sababu zingine, itachukuliwa kuwa ni ushahidi unaotosha kuwa mgombea amewasilisha taarifa. (Kifungu cha 9(3)).

## 6.0 MENEJIMENTI YA GHARAMA ZA UCHAGUZI

Kila mgombea, chama cha siasa, asasi ya kiraia au taasisi ya kidini iliyohusika katika shughuli za uhamasishaji na uelimishaji umma katika uchaguzi, inao wajibu wa kutunza taarifa za gharama za uchaguzi. (Kifungu cha 19 (1) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 13(3)).

Kila chama cha siasa kinapaswa kuwa na akaunti maalum ya benki kwa ajili ya gharama za uchaguzi, ambayo mapato na matumizi yote ya shughuli za uchaguzi yatafanywa kupitia akaunti hiyo. Hivyo, michango yote ya gharama za uchaguzi itakayopokelewa na chama itawekwa na kutumika kutoka katika akaunti hiyo (Kifungu cha 11 (2)).

Misaada yote itakayotolewa kwa ajili ya mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya chama au uchaguzi inapaswa kuwasilishwa kwa chama cha siasa husika na siyo vinginevyo. (Kifungu cha 15 (1)).

Mtu yeyote anayefanya malipo ya gharama za uchaguzi anapaswa kutoa stakabadhi au uthibitisho mwingine wowote wa malipo hayo. Kifungu cha (16).

Kwa idhini ya mgombea, Chama cha siasa kinaweza kutoa fedha



wa sheria, kitaruhusiwa kushiriki katika uchaguzi. (Kifungu 18(4)).

13.3 Asasi ya kiraia au taasisi ya kidini itakayoshindwa kuweka wazi chanzo na kiasi cha fedha kitakachotumika kwa ajili ya uhamasishaji na kutoa elimu kwa umma katika uchaguzi au kutumia zaidi ya ukomo uliowekwa kwa mujibu wa Sheria au itakayoshindwa ndani ya siku tisini (90) kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa taarifa ya fedha zilizotumika katika uchaguzi itakuwa imetenda kosa la jinai na ikitiwa hatiani itapewa adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni tano (5,000,000/=) au kifungo kisichozidi miaka mitatu (3) au adhabu zote mbili kwa pamoja. (Kifungu cha 13).

13.4 Mgombea aliyeshinda au kushindwa uchaguzi ambaye atashindwa kuandaa na kuwasilisha ripoti ya gharama za uchaguzi kwa chama kilichomdhamini ndani ya siku sitini (60) baada ya siku ya kupiga kura, atakuwa ametenda kosa la jinai na akitiwa hatiani atapewa adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni mbili (2,000,000/=) au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja. (Kifungu cha 18(5) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 18(1)).

13.5 Mtu atakayetumia au kutishia kutumia nguvu, vurugu, kujeruhi, kuharibu au kumdhuru mtu yoyote aliyechangia au anayetaka kuchangia fedha kwa mgombea au mwanafamilia wa mchangiaji au shughuli zake za kiuchumi, atakuwa ametenda kosa la jinai na akitiwa hatiani atapewa adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni moja (1,000,000/=) na isiyozidi shilingi milioni tano (5,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi sita (6) na kisichozidi miaka miwili (2) au adhabu zote mbili kwa pamoja. (Kifungu cha 11(5) na (7)).

13.6 Chama cha siasa, asasi ya kiraia au taasisi ya kidini au mwanachama wa taasisi hizo au mtu yoyote atakayeingiza nchini fedha kwa ajili ya gharama za uchaguzi ndani ya siku tisini (90) kabla ya uchaguzi na ndani ya siku thelathini (30) kabla ya uchaguzi mdogo atakuwa ametenda kosa la jinai na endapo atakutwa na hatia, kwa chama cha siasa kitapewa adhabu ya faini isiyozidi shilingi milioni tatu (3,000,000/=), kwa mgombea atapewa

majini, nauli ya treni au usafiri wa mnyama wa aina yoyote ile, kwenda au kutoka katika kituo cha kupiga kura. Aidha, mtu anayeruhusu, anayekodisha au anayetoa au mtu anayekodi, anayekopa au anayetumia gari, chombo cha majini, nauli ya treni au usafiri wa mnyama wa aina yoyote ile, kusafirisha wapiga kura kwenda au kutoka katika kituo cha kupiga kura naye amefanya kitendo kinachokatazwa. Isipokuwa kifungu hiki hakizuii mpiga kura au wapiga kura kwa gharama zao kukodi gari au chombo chochote kwenda au kutoka katika kituo cha kupiga kura.

x) **Kutumia nyumba, ardhi, jengo au eneo lolote kwa madhumuni ya kujitangaza ili kuteuliwa kuwa mgombea au kushinda uchaguzi (Kifungu 23(1)(b)**
Sheria inakataza mtu yoyote kufanya malipo kwa kuingia mkataba wa malipo na mpiga kura kwa ajili ya kutumia nyumba, ardhi, jengo au eneo kwa lengo la kujitangaza ili ateuliwe kuwa mgombea au ashinde uchaguzi.

Aidha, mtu yoyote atakayepokea malipo ya fedha au ambaye ni sehemu ya mkataba huo ambaye anafahamu kuwa kitendo hicho ni uvunjifu wa kifungu cha 23 naye anakuwa amefanya vitendo vinavyokatazwa (Kifungu 23 (2)).

## 13.0 ADHABU CHINI YA SHERIA YA GHARAMA ZA UCHAGUZI

13.1 Chama cha siasa au mgombea atakayeshindwa kuweka wazi kiasi na vyanzo vya fedha zinazopaswa kutumika kama gharama za uchaguzi anastahili kuenguliwa kushiriki katika uchaguzi.

13.2 Chama cha siasa kikishindwa kuwasilisha taarifa ya fedha na ripoti ya ukaguzi zinazohitajika kwa mujibu wa sheria kitapewa adhabu ya kulipa faini ya Shilingi milioni tatu (3,000,000/=), kutakiwa kuwasilisha nyaraka hizo na kupoteza sifa ya kushiriki katika uchaguzi. Endapo chama hicho kitawasilisha nyaraka hizo kabla ya siku ya uteuzi inayofuata, na Msajili akaridhika kwamba nyaraka hizo zimewasilishwa kama zinavyohitajika kwa mujibu



kugharamia matangazo na mikutano ya kampeni ya mgombea husika. Kifungu cha 17 (1).

Vilevile, misaada kutoka nje ya nchi inapaswa kupokelewa siku tisini (90) kabla ya uchaguzi mkuu na siku thelathini (30) kabla ya uchaguzi mdogo, lengo ni kuepusha fedha au kitu chochote cha thamani kutoka nje ya nchi kutumika kuvuruga uchaguzi. (Kifungu cha 12 (3) (a) na (b)).

## 7.0 TIMU YA KAMPENI

Timu ya kampeni maana yake ni kundi la watu lililoundwa na mgombea wakati wa mchakato wa uteuzi au uchaguzi kwa lengo la kumnadi na kumsaidia mgombea huyo katika kampeni za uchaguzi (Kifungu 7(3)).

Mgombea atakayekuwa na timu ya kampeni anapaswa kuwasilisha majina ya watu wanaounda timu yake ya kampeni siku mbili kabla ya kuanza kwa mchakato wa uteuzi au siku saba baada ya uteuzi, kama ifuatavyo:

1) Mgombea urais anapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa timu yake ya kampeni yenye watu wasiozidi hamsini (50). (Kanuni 17(1)(a));
2) Mgombea ubunge katika eneo la Tanzania Bara anapaswa kuwasilisha kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika timu yake ya kampeni yenye watu wasiozidi ishirini (20). (Kanuni 17(1)(b));
3) Mgombea ubunge katika eneo la Tanzania Zanzibar anapaswa kuwasilisha kwa Katibu Tawala wa Wilaya timu yake ya kampeni yenye watu wasiozidi ishirini (20). (Kanuni 17(1)(b)); na
4) Mgombea udiwani anapaswa kuwasilisha kwa Afisa Mtendaji Kata timu yake ya kampeni yenye watu wasiozidi kumi (10). (Kanuni 17(1)(c)).

Aidha, timu ya kampeni haitajumuisha mtu yeyote ambaye ni mwanakikundi wa kikundi cha uhamasishaji.
Asasi za kiraia na taasisi za kidini zitakazoshiriki katika kufanya uhamasishaji na kutoa elimu kwa umma zitapaswa kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa mpango kazi unaoeleza jinsi itakavyofanya uhamasishaji na uelimishaji umma kuhusu mchakato wa uteuzi wa

wagombea ndani ya vyama vya siasa, kampeni za uchaguzi au uchaguzi. Mpango kazi huo usitumike kubagua wagombea, chama cha siasa au kutumika kwa malengo mengine tofauti na uhamasishaji na uelimishaji umma. (Kanuni 12(2)(3) ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi 2010).

## 8.0 VIWANGO VYA GHARAMA ZA UCHAGUZI

Ili kuhakikisha kuna mazingira yaliyo sawa kwa wagombea, Sheria ya Gharama za Uchaguzi imeweka ukomo wa matumizi ya gharama za uchaguzi. Kwa mujibu wa kifungu cha 10 (1), Waziri mwenye dhamana hutoa tangazo katika Gazeti la Serikali linaloonesha ukomo wa matumizi ya gharama za uchaguzi kwa kila jimbo, mgombea urais, chama cha siasa, asasi za kiraia na taasisi za kidini zitakazofanya kazi ya kutoa elimu kwa umma wakati wa uchaguzi. Mgawanyo huo unafanywa kwa kuzingatia masuala yafuatayo:

1. Tofauti ya ukubwa wa eneo la jimbo;
2. Aina za wagombea;
3. Idadi ya watu katika jimbo; na
4. Miundombinu na mawasiliano.

Tarehe 19 Agosti, 2015 Waziri mwenye dhamana ya Vyama vya Siasa alitoa tangazo namba 325 katika Gazeti la Serikali Namba 6 linalohusu ukomo wa gharama za uchaguzi kama ifuatavyo:

1. Ukomo wa gharama za uchaguzi katika mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya chama cha siasa kama ifuatavyo:
   (i). Mgombea urais shilingi bilioni tatu(3,000,000,000/=);
   (ii). Wagombea ubunge shilingi bilioni tatu (3,000,000,000/=);
   (iii). Wagombea ubunge viti maalum vya wanawake shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=);
   (iv). Wagombea udiwani shilingi bilioni mbili (2,000,000,000/=);
   (v). Wagombea udiwani viti maalum vya wanawake shilingi milioni mia nne (400,000,000/=);
2. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa chama cha siasa katika kampeni za uchaguzi ni shilingi bilioni kumi na saba (17,000,000,000/=);
3. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea urais wa



fedha, ili zitumike kwa ajili ya hongo katika mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa na uchaguzi.

vi) **Kupokea au kukubali kupokea fedha, zawadi, mkopo, msaada, ahadi, wadhifa au kitu chochote chenye thamani ili upige au usipige kura. (Kifungu 21(1)(f)**
Sheria inakataza mtu yoyote, yeye mwenyewe au mtu mwingine kwa niaba yake, moja kwa moja au kwa namna nyingine yoyote, kupokea au kukubali kupokea au kuwa na mkataba wa kifedha, zawadi, mkopo, msaada, ahadi, ajira, wadhifa au kitu chochote chenye thamani, ili yeye mwenyewe au mtu mwingine apige au asipige kura.

vii) **Baada ya mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa au uchaguzi kupokea fedha au kitu cha thamani kutoka kwa mtu aliyepiga au ambaye hakupiga kura, baada ya kumshawishi kupiga au kutopiga kura (Kifungu 21(1)(g)**

Sheria inakataza mtu yoyote, yeye mwenyewe au mtu mwingine kwa niaba yake, moja kwa moja au kwa namna nyingine yoyote, baada ya mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa au uchaguzi, kupokea fedha au kitu cha thamani kutoka kwa mtu aliyepiga au ambaye hakupiga kura, baada ya kumshawishi kupiga au kutopiga kura.

viii) **Kwa njia ya rushwa, kutoa, kulipia au kupokea chakula, vinywaji, burudani ili kumshawishi mtu kupiga kura au kutopiga kura. (Kifungu 22 (a) na (b)**
Sheria inakataza mtu yoyote, yeye mwenyewe au mtu mwingine kwa niaba yake, kabla, wakati au baada ya mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa au uchaguzi, moja kwa moja au kwa namna nyingine yoyote, kwa njia ya rushwa, kutoa, kulipia au kupokea chakula, vinywaji au burudani ili kumshawishi mtu kupiga kura au kutopiga kura.

ix) **Kulipa au kuingia mkataba wa kulipia kusafirisha wapiga kura (Kifungu 23(1)(a), (3), (4) na (5)**
Sheria inakataza mtu yoyote, kulipa au kuingia mkataba wa kulipia usafiri wa wapiga kura au kukodisha gari, chombo cha

na wakati wa mchakato wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama vya siasa kwa mtu aliyetangaza au kufanya vitendo vinavyoonesha nia ya kushiriki katika mchakato wa uteuzi, wakati wa uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi na uchaguzi.

**i) Kutoa Fedha, Mikopo au kitu chochote chenye thamani ili kupigiwa kura (Kifungu 21(1)(a)**

Sheria inakataza mgombea, wakala au chama cha siasa kutoa moja kwa moja au kwa namna nyingine yoyote, fedha, mkopo, ahadi ya fedha au kitu chochote chenye thamani ili kumrubuni mtu kupiga kura, kuacha kupiga kura au kufanya kitendo chochote kinachohusiana na mchakato wa uchaguzi.

**ii) Kuahidi au kutoa ajira, wadhifa sehemu ya kazi ili kupigiwa kura (Kifungu 21(1)(b)**

Sheria inakataza mtu yoyote kuahidi kutoa, kutoa ajira au wadhifa sehemu ya kazi kwa mpiga kura au mtu mwingine kwa niaba ya mpiga kura au kwa chama chake, ili kumshawishi mpiga kura huyo kupiga kura au kuacha kupiga kura katika uchaguzi wowote.

**iii) Kutoa zawadi, mkopo, msaada, ahadi, kununua kitu chochote au kuingia makubaliano na mtu mwingine, ili kupata uteuzi (Kifungu 21(1)(c).**

Sheria inakataza mtu yoyote, wakala wake au kupitia chama chake, kutoa moja kwa moja au kwa njia yoyote ile zawadi, mkopo, msaada, ahadi, kununua kitu chochote au kuingia makubaliano na mtu mwingine, ili kupata uteuzi.

**iv) Kutoa au kuwezesha kupatikana kwa uteuzi kutokana na zawadi, mkopo, msaada, ahadi au makubaliano yaliyoingiwa (Kifungu 21(1)(d)**

Sheria inakataza mtu yoyote kupata, kuahidi au kumwezesha mtu kupata uteuzi kuwa mgombea katika chama cha siasa, kutokana na zawadi, mkopo, ahadi, msaada, kununua au kwa makubaliano.

**v) Kulipa au kuwezesha kulipwa fedha ili zitumiwe kwa ajili ya hongo (Kifungu 21(1)(e)**

Sheria inakataza mtu yoyote kulipa au kuwezesha kulipwa



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni shilingi bilioni sita (6,000,000,000/=);

4. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea wa ubunge katika jimbo la uchaguzi umeanishwa katika sehemu B ya tangazo, ambapo kila jimbo lina ukomo wake;
5. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea wa kiti maalum cha ubunge ni shilingi milioni kumi na moja (11,000,000/=);
6. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea udiwani ni shilingi milioni nane (8,000,000/=) kwa kata ya mjini na milioni sita (6,000,000/=) kwa kata za vijijini;
7. Ukomo wa gharama za uchaguzi kwa mgombea udiwani viti maalum, kwa kata ya mjini ni shilingi milioni nne (4,000,000/=) na kwa kata ya kijijini ni shilingi milioni tatu na nusu (3,500,000/=); na
8. Kwa upande wa asasi za kiraia na taasisi za kidini zitakazoshiriki katika kufanya uhamasishaji na kutoa elimu kwa umma, ukomo wa matumizi wa gharama za uchaguzi zitakua kama ifuatavyo: (Kanuni ya 12(1) ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi).

(i) Kwa asasi itakayoshiriki nchi nzima ukomo wake utakuwa shilingi bilioni moja (1,000,000,000/=);

(ii) Kwa asasi itakayoshiriki katika ngazi ya jimbo ukomo wake utakuwa shilingi milioni mia moja (100,000,000/=); na

(iii) Kwa asasi itakayoshiriki katika ngazi ya kata ukomo wake utakuwa shilingi milioni kumi (10,000,000/=).

Gharama zote za uchaguzi zitakazotumika wakati wa uteuzi wa wagombea ndani ya chama cha siasa zitatokana na chama husika. (Kifungu cha 14(1)).

Chama cha siasa au mgombea atakayetumia gharama za uchaguzi zaidi ya ukomo uliowekwa anapaswa kutoa taarifa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa akieleza sababu za kufanya hivyo (Kifungu cha

10(2)). Aidha, mgombea au chama cha siasa hakipaswi kutumia zaidi ya asilimia kumi na tano (15%) ya gharama za uchaguzi zinazopaswa kutumika katika eneo husika (Kanuni ya 3 ya Amri za Gharama za Uchaguzi Namba 325 za mwaka 2015).

## 9.0 MGAWANYO WA MATUMIZI BAINA YA CHAMA NA MGOMBEA

Sheria ya Gharama za Uchaguzi katika kifungu cha 17(1) inaruhusu mgawanyo wa gharama za uchaguzi zilizotumika na mgombea mwenyewe na zile ambazo chama kimetumia kumtangaza mgombea pamoja na mikutano yote. Kwa hali hiyo chama kitafanya yafuatayo:

1. Kuweka mgawanyo ulio wazi baina ya matumizi ya mgombea kadiri itakavyowezekana na yale yaliyofanywa na chama.
2. Ndani ya siku thelathini (30) baada ya kupiga kura chama kitamjulisha mgombea kiasi cha gharama za uchaguzi alichotengewa na chama ambacho kitakuwa ni sehemu ya gharama za uchaguzi za mgombea.

## 10.0 MAREJESHO YA GHARAMA ZA UCHAGUZI

Mgombea anapaswa kuandaa, kuhakiki na kuwasilisha kwa kutumia fomu EE.11 ripoti ya gharama za uchaguzi alizotumia wakati wa kampeni na uchaguzi, ndani ya siku sitini (60) tangu apewe taarifa ya fedha alizotengewa na chama chake kwa ajili ya gharama za uchaguzi. Kwa upande wa mgombea urais atawasilisha kwa Katibu Mkuu wa Chama chake, na kwa mgombea ubunge au udiwani atawasilisha kwa mtu anayetekeleza majukumu ya Katibu Mkuu ndani ya Wilaya husika (Kifungu cha 18 cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi kikisomwa pamoja na Kanuni ya 15 ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi.

Baada ya kupokea taarifa kutoka kwa mgombea, Katibu Mkuu wa chama ataihakiki na kuiwasilisha kwa Bodi ya wadhamini wa chama chake ambayo itawasilisha ripoti hiyo kwa Msajili wa Vyama vya Siasa kwa kutumia fomu namba EE.12. (Kanuni 15(5) ya Kanuni za Gharama za Uchaguzi).

Kila chama cha siasa ambacho kimeweka mgombea, kinapaswa ndani ya siku mia moja na themanini (180) baada ya mgombea



wake kuwasilisha ripoti ya matumizi ya gharama za uchaguzi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ripoti ya matumizi ya fedha yanayomhusu mgombea husika kwa kutumia fomu namba EE.12 ikiambatana na stakabadhi au ushahidi wowote wa malipo yaliyofanyika. Aidha, ripoti ya chama itajumuisha masuala yafuatayo:

1) Ripoti ya fedha ya gharama za uchaguzi;
2) Hesabu ya fedha zote zilizopokelewa na kutumika na mgombea au mtu yoyote kwa niaba ya mgombea kwa madhumuni ya gharama za uchaguzi na ieleze kila malipo yaliyofanyika na vyanzo vya mapato hayo;
3) Maelezo ya mgombea yanayothibitisha kwamba hakuna malipo yaliyofanyika ambayo hayakuidhinishwa na sheria na iaminike kwamba kila gharama zilizotumika zimejumuishwa katika ripoti ya chama chake; na
4) Ripoti ya ukaguzi kama inavyohitajika na sheria hii.

Kwa upande wa asasi za kiraia na taasisi za kidini ambazo zimeshiriki katika uchaguzi kufanya uhamasishaji na kutoa elimu kwa umma, kila asasi/taasisi inapaswa kuwasilisha ripoti ya gharama za uchaguzi kwa kujaza fomu namba EE.13. Kanuni 15(7) ya kanuni za gharama za uchaguzi. Ripoti hiyo inapaswa kuwa na masuala yafuatayo:

(i) Hesabu au gharama zilizotumika;
(ii) Hesabu ya fedha zilizopokelewa; na
(iii) Ankara na stakabadhi za malipo.

## 11.0 UKAGUZI WA GHARAMA ZA UCHAGUZI

Kifungu cha 19(4) kinaeleza kuwa taarifa zote za gharama za uchaguzi zinapaswa kukaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

## 12.0 VITENDO VINAVYOKATAZWA

(Sehemu ya tano (5) ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi)

Sheria ya Gharama za Uchaguzi inakataza vitendo vifuatavyo kabla